# MAOMBI YA MAPINDUZI

**JUSTICE B. LUTASHOBYA**

***"Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, AKAZIPINDUA meza za wabadili fedha, na viti vyao waliokuwa wakiuza njiwa." [ MATHAYO 21:12]***

***Yohana 16: 24 " Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; OMBENI, nanyi mtapata; FURAHA YENU IWE TIMILIFU"***

***" Basi Yesu aliwaambia tena, Amini, amini nawaambieni, Mimi ndimi MLANGO wa kondoo. Wote walionitangulia ni wezi na wanyang'anyi, lakini kondoo hawakuwasikia. Mimi ndimi MLANGO; mtu akiingia kwa mimi, ATAOKOKA, ataingia na kutoka, naye atapata malisho." [YOHANA 10: 7-9]***

# MAOMBI YA MAPINDUZI

*Copyright 2012: Mchungaji Justice B.Lutashobya*

*Kimechapwa Tanzania*
*Na: LIBERTY MEDIA CO. LTD*
*Cell: +255 767 599958 / 713 500044 / 717 599958*
*email: liberty.co12@gmail.com*
*Dar es salaam*

*Chapa ya kwanza mwaka 2012:*

*Haki zote zimehifadhiwa*
*Hairuhusiwi kunakili kitabu hiki*
*kwa namna zozote bila ruhusa ya Mwandishi*
*kwa ajili ya kuuza au kufanyia biashara.*

*Lakini unaruhusiwa kunakili*
*Sehemu tu ya ujumbe katika kitabu hiki*
*Kwa ajili ya Kushuhudia, kuhubiri na kufundisha wakristo*
*Na wasio wakristo, kanisa lolote, shule za jumapili, shule za huduma, Mikutano ya injili, semina ya neno la Mungu na madarasa ya maombi.*

*Kwa mawasiliano zaidi,Tuandikie kwa anwani hii ifuatayo:*

*Justice na Adeline Lutashobya*
*World Miracle Mission Center*
*P.o Box 78620*
*Dar es salaam*

*Cell: +255 754 -69 20 19 / 754-470 924 / 715- 470 924,*

*Email: pastorjustice@gmail.com  au info@wmmctz.org*
*Web1: www.wmmctz.org*
*Web 2: www.blessingcommunity.org*

*Maandiko yote ni kutoka katika Biblia tafsiri ya Union version, isipokuwa kama imetajwa vinginevyo.*



# SHUKRANI

Mungu wa Mbinguni, ninakushukuru katika Jina la Yesu na la Roho Mtakatifu aliyenihuisha kuandika kitabu hiki kwa watu wako uliowaumba kwa mfano wako. Ufalme wako uje juu ya watu wako kupitia Neno lako lililotumwa kwao ili kuwaokoa na kuwaponya kutoka maangamizo yao. Ushuhuda wa Injili ya Yesu Kristo kwa ufunuo, ushauri , mafundisho na kumbukumbu za Roho Mtakataifu ndiyo uliyofanikisha maandalizi ya kitabu hiki katika nafasi ya kwanza. Heshima na Utukufu namrudishia BWANA WA MAJESHI KATIKA KITI CHA ENZI.

Pili natoa shukrani kwa Mke wangu mpendwa Adeline Lutashobya kwa kujitolea kwake kuhakiki kitabu hiki kama mhariri, ikaongozwa na Roho Mtakatifu. Ahsante kwa maombi ya mapinduzi uliyofanya kuhakikisha kitabu hiki kinatoka katika uvuvio wa Roho Mtakatifu.

Tatu nawashukuru  shemeji yangu Anchila na watoto wangu wapendwa, Jesse, Joyous na Namala ambao waliendelea kuiombea kazi hii ya mapinduzi, kuhakikisha inatunzwa. Mungu wa Mbingu awafungulie Milango 12 ya mapinduzi katika maisha yenu.

Nne, Namshukuru Maro Nyamate aliyetoa ushauri wa kina katika haki za kitabu hiki, pamoja na sadaka ya muda wake kuunda tovuti na barua pepe za huduma ya WMMC  na BLESSING COMMUNITY. Mwisho namshukuru Robert Mwasongwe ambaye amesaidia kutengeneza sehemu ya jarada ya kitabu hiki pamoja na kukipanga katika mfumo wa kutolewa chapa.

**NEEMA YA BWANA WETU YESU KRISTO,  NA UPENDO WA MUNGU BABA, NA USHIRIKA WA ROHO MTAKATIFU, UWE PAMOJA NASI SOTE , SASA NA HATA MILELE. AMINA**

## YALIYOMO

**SHUKRANI ................................................................III**
Utangulizi.......................................................................VII
Mapinduzi ni nini? [ MATH21: 12-15]..........................VII

**SURA YA KWANZA ........................................................ 1**
Mapinduzi ni Nini? ........................................................ 1
Mapinduzi ni nini? ......................................................... 1
Aina za Mapinduzi .......................................................... 4
Wokovu ni mapinduzi ...................................................... 9
Miujiza na ishara ni Mapinduzi ..................................... 11

**SURA YA PILI ............................................................. 17**
Mapinduzi katika Maombi ............................................ 17
Kusudi la Maombi ya Mapinduzi .................................. 19
Jeshi la Maombi ya Mapinduzi ...................................... 22
Moyo wa Maombi juu ya Nchi ...................................... 23

**SURA YA TATU........................................................... 25**
Wanamapinduzi wa Maombi ......................................... 25

**SURA YA NNE............................................................. 39**
Roho za kupinduliwa ..................................................... 39
Roho za tunutu .............................................................. 39
Roho za Nzige................................................................ 41
Roho za Parare .............................................................. 43
Roho za madumadu........................................................ 43
Mapinduzi ya Ninawi..................................................... 44
Urejesho baada ya Mapinduzi....................................... 44

**SURA YA TANO ................................................................ 47**
Mkutano wa Maombi ..................................................... 47
Mkutano wa Maombi juu ya Nchi ya Tanzania ............. 48
Mapinduzi ya kiroho yanakuja Tanzania ....................... 49

**SURA YA SITA .................................................................... 53**
Dhabihu ya Maombolezo ............................................... 53
Tunahitaji Sadaka ya Maombolezo siyo Fedha. ............. 56

**SURA YA SABA.................................................................. 59**
Kupanua hema la Maombi ............................................. 59
Maandalizi ya Kuingia Hema la Maombi ....................... 63
Maombolezo Juu ya Nchi .............................................. 64

**SURA YA NANE ................................................................ 67**
Milango 12 ya Mapinduzi .............................................. 67
Yesu ni Mlango mkuu ................................................... 68
Milango mitatu ya Kiroho.............................................. 69
Milango ya Mbinguni .................................................... 70
Milango ya Duniani ....................................................... 73
Milango ya Kuzimu ...................................................... 74
Milango 12 ya Mapinduzi 2012..................................... 75

**TAMATI ............................................................................. 76**



# UTANGULIZI

Amani ya Kristo iwe kwako ndugu mpendwa, Karibu katika semina ya neno la Mungu kwa njia ya kitabu hiki. Nafahamu umekuwa ukisikia habari nyingi kuhusu Maombi labda kupitia semina, mkutano wa njili, kanisani, au hata katika mitandao mbalimbali ya kiroho. Lakini mimi nakuletea habari za maombi ya mapinduzi ambayo unaweza kuyatumia kama silaha kufanya mapinduzi katika ulimwengu wa roho na mwili. Kuna roho zidanganyazo ambazo zimekuwa tanzi katika maisha yako ya kiroho na kimwili. Hizi ndizo zinazozuia maendeleo yako kiroho, kuhudumia, kikazi, kifamilia, kifedha, kijamii na hata kitaifa.

Mwandishi wa kitabu hiki anakushirikisha jinsi ya kupambana na Roho za ZA TUNUTU, NZIGE, PARARE NA MADUDU ambazo zimetafuna watoto wako, baba yako, mama yako, mume wako, bosi wako, mjomba wako, mtaa wako, kijiji chako, kata yako wilaya yako, mkoa wako na taifa lako. Zipo roho za tunutu, nzige, parare na madumadu ambazo zimelitafuna taifa na mali zote zimepotea. Huu ni mtandao wote, ni jamii moja ya panzi. Unaweza kufikiri ni chama hiki cha siasa labda ndicho kitaleta mapinduzi katika nchi ya Tanzania kumbe tunutu; Unaweza ukafikiri labda ni chama cha upinzani kitaleta mabadiliko kumbe ni nzige; Unaweza kuwa labda chama cha kabila fulani kumbe ni parare; na labda chama cha zanzibar kumbe ni madumadu.

## Mapinduzi ni nini? [ MATH21: 12-15]

Mapinduzi ni neno la kiswahili linalomaanisha MAGEUZI, kutoka hali au nafasi fulani ambayo haiwapendezi jamii ya watu. Haya ni mapinduzi ya Kimwili. Kusudi la mapinduzi haya inaweza kuwa watu hawa wanataka mabadiliko katika nchi yao au jamii yao. Watu hawa wanatawaliwa na roho ya mapinduzi na mara nyingi wanaweza kuunda chama au jeshi la kufanya mapinduzi. Wapo wanaharakati wa mapinduzi, ambao wanaitwa wanamapinduzi. Mapinduzi yanayofanyika yawe ya Kidemokrasia

au ya Kijeshi yanalenga kupata uhuru na kuleta furaha katika ile jamii iliyopanga kufayafanya. Kawaida ya mwanadamu anapochoka na hali fulani ambayo hairidhishi nafsi yake hupenda mabadiliko.

Tanzania sasa tunahitaji mapinduzi katika ulimwengu wa roho na mwili, kwa sababu watu hawana amani na furaha iliyotimilifu. Ndiyo maana mwandishi wa kitabu anasisitiza kufanya maombi ya mapinduzi ya kiroho. Kama ilivyoandikwa katika Yohana 16: 24 " **Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; OMBENI, nanyi mtapata; FURAHA YENU IWE TIMILIFU"**. Furaha ya watanzania kwa sasa siyo timilifu kwa sababu ya utaratibu wa mifumo mibaya ya maisha ya watanzania. Mifumo iliyojaa dhuluma, rushwa, ufisadi, ubinafsi, uchawi, ushirikina na uovu wa kila namna. Mifumo mingi ya nchi yetu sasa haina moyo wa taifa; moyo wa kujali masilahi ya taifa, mali za taifa, haki ya kitaifa na upendo wa kitaifa. Ukitazama nchi kama Marekani, wanao moyo na upendo wa nchi yao, wanajali wananchi wao kwa upendo na mshikamano mkubwa. Ukitaka kujua jinsi ambavyo wanajali wananchi wao, tazama mmarekani mmoja anapopatwa na mkasa wowote duniani. Marekani inatuma msaada wa haraka sana wa kumhudumia mmarekani mmoja. Viongozi wanalipa gharama kubwa kuhakikisha wanamwokoa mmarekani mmoja ambaye yuko hatarini. Na kutoa ni moyo siyo utajiri, kama mithali ya kiswahili isemavyo. Ujumbe wangu katika kitabu hiki unalenga kurejesha MOYO WA TAIFA KWA WATANZANIA. Kwa kiingereza, Spirit of a Nation. Mungu amenipa ujumbe huu KUPINDUA MOYO WA UTENGANO ILI KUJENGA MOYO WA KITAIFA. Biblia inasema jitenge na mtu asiyetembea katika utaratibu. Biblia inaendelea kusisitiza katika kitabu cha Mithali 28:9 ya kwamba Yeye aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria, hata sala yake ni chukizo. Hili ni tatizo linaloonekana katika jamii ya watanzania na jitihada za kutafuta MILANGO ya kutokea kwa njia zote za kidemokrasia na kijeshi zimeshindwa kuleta suluhisho. Basi kunahitajika MLANGO WA THEOKRASIA. Mara nyingi Mungu anapenda apewe utukufu katika tatizo linapojitokeza. Theokrasia ni mlango wa KIMUNGU unatumiwa na Mungu mwenyewe na watu wanaomwabudu katika roho na kweli ili kuufungua kwa ajili ya kuwaokoa watu wote.

Mzigo wa maombi ya mapinduzi umejengeka kwangu toka mwezi Juni, 2011 nilipofanya mapinduzi katika maombi yangu. Badala ya kuomba kwa ajili huduma yangu na familia, sasa nikafunga muda wa miezi saba na kuanza kufanya maombi ya usiku. Safari hii nilikuwa nafunga na kuomba usiku kuanzia saa tano usiku kila siku hadi saa nane au tisa wakati mwingine. Maombi ya mapinduzi juu ya TAIFA, KABILA NA LUGHA yalitawala na yanaendelea kutawala moyo wangu.Nilishangaa siku kwa siku katika kipindi hicho cha maombi haya, naomboleza sana kwa machozi juu ya Wizara, taasisi za elimu, matibabu, huduma za jamii, programu za kijamii, raisi wa nchi, mawaziri, wabunge, madiwani, mitaa, vitongoji, vijiji, kata, tarafa, wilaya, mikoa, manispaa, miji kabila mbali mbali Tanzania. Wakati huu Mungu alipindua maombi yangu ya kawaida niliyozoea kufanya. Kamwe hakuniruhusu kuomba jinsi nilivyozoea. Kila nikikaa kwenye kiti nalipuka kama baruti na mabom makali sana, baadaye Roho Mtakatifu alikuwa akininongoneza kwa sauti ya ndani, MAPINDUZI YANAENDELEA! Moyo wangu hata sasa ninapokuletea habari hizi unalipuka juu maombi ya mapinduzi kwa ajili ya Tanzania.

Toba juu Taifa, Kabila na lugha zilitawala maombi yangu ya mapinduzi. Nilisitukia napiga kelele BABA PINDUA TATIZO HILI, PINDUA LA PILI, PINDUA UOVU, PINDUA DHAMBI HII, PINDUA LAANA KATIKA JINA LA YESU! Mambo mengi niliyoomba wakati wa mapinduzi katika kuomba kwangu, yamepinduliwa. Na hata wewe unayesoma kitabu hiki, yako mambo yanayokwenda kupinduliwa , zipo roho zilizotafuna maisha yako zitapinduliwa, mapepo yaliyotumwa kutoka kuzimu yatapinduliwa, wako maadui wako nao watapinduliwa katika maombi ya mapinduzi; yako mapinduzi ya kifedha yatakayofanyika juu yako kuanzia sasa unaposoma kitabu hiki; utaanza kusikia chemi chemi ya roho ya maombi ya mapinduzi; usijizuie kama unasikia machozi lia kwa sauti kuu! Kama unasikia kunena kwa lugha nena kwa lugha! Kama unasikia tetemeko ndani ya roho yako kaa katika uwepo wa maombi ya

tetemeko! Kama unasikia maombolezo omboleza usinyamaze! Kama unasikia kuimba maombi ya mapinduzi utakayopewa imba kwa sauti kuu! Kumbuka Mfalme Yehoshafati alivyopindua maadui wa Israel kwa kilele za sifa za maombi ya mapinduzi. Anza kujifunza mapinduzi ya maombi yako, Unaweza kuimba maombi, unaweza kunena maombi, unaweza kusifu katika maombi, unaweza kupiga kelele katika maombi, unaweza kufunga katika maombi, unaweza kupangilia maombi, unaweza kuteka nyara katika maombi, unaweza kufanya kazi katika maombi, unaweza kuendesha katika maombi, unaweza kulala katika maombi, unaweza kulima shamba lako katika maombi. Enyi walinzi wa Yerusalemu msinyamaze hadi Yerusalemu itakapofanywa imara [ ISAYA 62: 6-7]

Kanisa la Mungu amka tufanye mapinduzi kwa sababu tunalo agizo. Tanzania bila kufanywa imara kiroho, ina maana tunahitaji roho ya mapinduzi. Mlango wa mapinduzi tumepewa na ufunguo wa mlango tumepewa. Bwana Yesu anatusubiri tufungue mlango huu apate kuingia Tanzania. Ndiyo maana anasema, Tazama nasimama mlangoni ukiufungua ataingia kufanya makao na kula pamoja na wewe; soma tena UFUNUO 3:20. Ipo milango 12 ya mapinduzi ambayo inalipasa kanisa lifungue ili Mungu apate kuingilia kati juu ya nchi, kabila na lugha za Tanzania.

Unapoendelea na kitabu hiki jinsi utakavyokuwa unageuza kurasa za kitabu hiki, ndivyo Mungu atakavyokuwa anageuza maisha yako. Atakuwa anajenga mahali palipobomoka; Mungu atakuwa anasawazisha palipokwaruzika; atakuwa anabomoa palipojengwa kwa makosa; atakuwa anarudisha vitu vilivyopotea wakati wa vita yako ya muda mrefu; atakuwa akishughulikia mapinduzi ya mateso yako kuwa furaha, atakuwa akifanya mapinduzi ya misiba kuwa arusi yako; atakuwa akigeuza umasikini wako kuwa utajiri; atakuwa akigeuza ugonjwa uliokutesa kwa muda mrefu kuwa afya njema; atakuwa akigeuza ujinga wako kuwa elimu; atakuwa akigeuza maisha magumu uliyonayo kuwa furaha, atageuza hukumu zako kuwa Wokovu, atageuza migogoro uliyonayo kuwa amani na maelewano; atapindua maadui zako; atapindua magari na vifaru vinavyokufuatilia nyuma yako bila kujua; ataondosha upepo katika magurudumu ya magari ya adui anayekufuatilia katika JINA LA YESU ! AMINA!

Kumbuka, alivyofanya kwa Musa na wana wa Israeli baada ya Maombi ya mapinduzi ya Musa nabii wa Bwana. Biblia inasema hivi:

***" Ikawa katika zamu ya alfajiri, Bwana akalichungulia jeshi la Wamisri katika ile nguzo ya moto na ya wingu, akalifadhaisha jeshi la Wamisri. Akayaondoa magurudumu ya magari yao, hata yakaenda kwa uzito; na Wamisri wakasema, Na tukimbie mbele ya Israeli; kwa kuwa Bwana anawapigania, kinyume cha Wamisri. [ KUTOKA 14:24-25]***

Mlango huu wa Mapinduzi kama haya yaliyofanyika ndiyo mwandishi anayoita Mapinduzi ya Theokrasia. Yalifanywa na Mungu mwenyewe kwa kutumia Maombi ya Mapinduzi. Wana wa Israeli walifungulia mlango wa maombi ya mapinduzi, naye Bwana akaingilia katika mlango huu wa mapinduzi. Mungu anayo milango mingi anayoingilia kutenda miujiza na ishara ili kufanya mapinduzi katika maisha ya mwanadamu. Lakini Mlango mmoja wapo aliotupa wakristo ni mlango wa maombi. Ili Kanisa lipate kufanya mapinduzi ya Kiroho na Kimwili katika Familia, Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, mkoa na Taifa kwa ujumla linatakiwa kuomba Bwana afungue milango 12 ya kufanya mapinduzi. Maombi ya mapinduzi hayawezi kufanyika bila kubadilisha maombi. Lazima maombi ya mapinduzi yafanyike kwa kufanya mapinduzi ya maombi; kwa maana ukitaka maombi yako yafanye mapinduzi, lazima upindue kwanza maombi ya mazoea. Ni wakati wa kubadilisha silaha ya kawaida ila kutumia sasa silaha ya mapinduzi. Safari hii maombi ya kupindua roho za tunutu, parare, madumadu na nzige ni masafa marefu. Kwa lugha ya kivita, silaha hii ndiyo wanasema lazima kutumia " LONG RANGE"; ili uweze kumlipua adui kutoka mafichoni na kisha kusambaratisha mtandao wake; ndipo mtaingia kuteka nyara na kutangaza mapinduzi ya utawala wa shetani.

# SURA YA KWANZA

## MAPINDUZI NI NINI?

***"Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, AKAZIPINDUA meza za wabadili fedha, na viti vyao waliokuwa wakiuza njiwa. akawaambia imeandikwa, nyumba yangu itaitwa nyumba ya Sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi. Na vipofu na viwete wakamwendea mle hekaluni, AKAWAPONYA. Lakini wakuu wa makuhani na waandishi walipoyoana maajabu aliyoyafanya, na watoto waliopaza sauti zao hekaluni, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi! walikasirika."***
***[ MATHAYO 21: 12-15]***

## Mapinduzi ni nini?

Mapinduzi ni neno la kiswahili linalomaanisha MAGEUZI, kutoka hali au nafasi fulani ambayo haiwapendezi jamii ya watu. Kubadilisha utaratibu wa mfumo mbaya wa maisha kwenda katika mfumo mzuri wa maisha. Haya ni mapinduzi ya Kimwili. Kusudi la mapinduzi haya inaweza kuwa watu hawa wanataka mabadiliko katika nchi yao au jamii yao. Watu hawa wanatawaliwa na roho ya mapinduzi na mara nyingi wanaweza kuunda chama au jeshi la kufanya mapinduzi. Wapo wanaharakati wa mapinduzi, ambao wanaitwa wanamapinduzi. Mapinduzi yanayofanyika yawe ya Kidemokrasia au ya Kijeshi yanalenga kupata uhuru na kuleta furaha katika ile jamii iliyopanga kuyafanya. Kawaida ya mwanadamu anapochoka na hali fulani ambayo hairidhishi nafsi yake hupenda mabadiliko. Unaweza kuona mapinduzi yaliyofanyika katika nchi za kiarabu hivi karibuni jinsi ambavyo mapinduzi yana gharama kubwa kwa jamii au taifa. Tumeshuhudia mapinduzi ya Tunisia, Libya, Misri na sasa Siria yalifanyika kwa nguvu ya kijeshi; lakini yamegharimu viongozi wa siasa kufa pamoja na baadhi ya wananchi.

Kila mtu aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu anatamani mabadiliko ya kimwili na kiroho. Tanzania sasa tunahitaji mapinduzi katika ulimwengu wa roho na mwili, kwa sababu watu hawana amani na furaha iliyotimilifu. Lakini hatuhitaji kufanya mapinduzi kama Tunisia, Libya, Misri wala Siria; bali kwa silaha za rohoni; maana vita vyetu si vya damu na nyama, bali ni katika ulimwengu wa roho. Ndiyo maana mwandishi wa kitabu anasisitiza kufanya maombi ya mapinduzi ya kiroho. Kama ilivyoandikwa katika Yohana 16: 24 " Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; OMBENI, nanyi mtapata; FURAHA YENU IWE TIMILIFU. Furaha ya watanzania kwa sasa siyo timilifu kwa sababu ya utaratibu wa mifumo mibaya ya maisha ya watanzania. Mifumo iliyojaa dhuluma, rushwa, ufisadi, ubinafsi, uchawi, ushirikina na uovu wa kila namna. Mifumo mingi ya nchi yetu sasa haina moyo wa taifa; moyo wa kujali masilahi ya taifa, mali za taifa, haki ya kitaifa na upendo wa kitaifa. Ukitazama nchi kama Marekani, wanao moyo na upendo wa nchi yao, wanajali wananchi wao kwa upendo na mshikamano mkubwa. Ukitaka kujua jinsi ambavyo wanajali wananchi wao, tazama mmarekani mmoja anapopatwa na mkasa wowote duniani. Marekani inatuma msaada wa haraka sana wa kumhudumia mmarekani mmoja. Viongozi wanalipa gharama kubwa kuhakikisha wanamwokoa mmarekani mmoja ambaye yuko hatarini. Na kutoa ni moyo siyo utajiri, kama mithali ya kiswahili isemavyo. Ujumbe wangu katika kitabu hiki unalenga kurejesha MOYO WA TAIFA KWA WATANZANIA. Kwa kiingereza, Spirit of a Nation. Mungu amenipa ujumbe huu, KUPINDUA MOYO WA UTENGANO ILI KUJENGA MOYO UMOJA WA KITAIFA. Biblia inasema jitenge na mtu asiyetembea katika utaratibu. Biblia inaendelea kusisitiza katika kitabu cha Mithali 28:9 ya kwamba, Yeye aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria, hata sala yake ni chukizo. Hili ni tatizo linaloonekana katika jamii ya watanzania na jitihada za kutafuta MILANGO ya kutokea kwa njia zote za kidemokrasia na kijeshi zimeshindwa kuleta suluhisho. Basi kunahitajika MLANGO WA THEOKRASIA. Mara nyingi Mungu anapenda apewe utukufu katika tatizo linapojitokeza. Theokrasia ni mlango wa KIMUNGU unaotumiwa na Mungu mwenyewe na watu wanaomwabudu katika roho na kweli ili kuufungua kwa ajili ya kuwaokoa watu wote.

Mzigo wa maombi ya mapinduzi umejengeka kwangu toka mwezi Juni, 2011 nilipofanya mapinduzi katika maombi yangu. Badala ya kuomba kwa ajili huduma yangu na familia, sasa nikafunga muda wa miezi saba na kuanza kufanya maombi ya usiku kwa ajili ya Tanzania. Safari hii nilikuwa nafunga na kuomba usiku kuanzia saa tano usiku kila siku hadi saa nane au tisa wakati mwingine. Maombi ya mapinduzi juu ya TAIFA, KABILA NA LUGHA yalitawala na yanaendelea kutawala moyo wangu. Nilishangaa siku kwa siku katika kipindi hicho cha maombi haya, naomboleza sana kwa machozi juu ya Wizara, taasisi za elimu, matibabu, huduma za jamii, programu za kijamii, raisi wa nchi, mawaziri, wabunge, madiwani, mitaa, vitongoji, vijiji, kata, tarafa, wilaya, mikoa, manispaa, miji kabila mbali mbali za Tanzania. Wakati huu Mungu alipindua maombi yangu ya kawaida niliyozoea kufanya. Kamwe, hakuniruhusu kuomba jinsi nilivyozoea. Kila nikikaa kwenye kiti nililipuka kama baruti na mabomu makali sana, baadaye Roho Mtakatifu alikuwa akininong'oneza kwa sauti ya ndani, MAPINDUZI YANAENDELEA! Moyo wangu hata sasa ninapokuletea habari hizi unalipuka juu maombi ya mapinduzi.

Katika neno letu la msingi hapo Mwanzo, tumeona jinsi ambavyo Bwana Yesu alipindua meza za wafanyabiashara wa fedha ndani ya hekalu, kisha akatangaza matumizi ya hekalu " akawaambia imeandikwa, nyumba yangu itaitwa nyumba ya Sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi." Bila shaka ukitafsiri zaidi alikuwa anawaambia natangaza mapinduzi ya biashara kichaa zinazofanyika katika Nyumba ya Mungu. Hivi kanisa la Kristo kuna biashara kichaa nyingi zinafanyika ambazo zinahitaji mzigo wa maombi ya mapinduzi. Mapinduzi yanaandaliwa kwenye maombi, kisha ndipo unaweza kwenda kuipindua dhambi na uovu sasa ambao umebisha hodi na kuingia makanisani. Mchungaji wangu, huu ni mzigo mkubwa sana kama umeitwa kwa ajili ya huduma yako. Fanya maombi ya Toba juu Kanisa, Taifa, Kabila na lugha ili

dhambi na uovu upinduliwe. Ikulu ya taifa ni sehemu ya madhabahu ya Bwana katika nchi ya Tanzania; ni nyumba ya Bwana; na sasa biashara kichaa zinaendelea kufanyika. Lazima Bwana Yesu atashuka, kupindua meza za wafanya biashara ndani ya ikulu ya taifa! Lazima mapenzi ya Bwana yatatimia!

Bwana Yesu alitangaza mapinduzi kutoka mbinguni, manabii walitangaza mapinduzi kabla Yesu hajazaliwa. Ninaposoma kitabu cha ufunuo sura ya 12 kuanzia mstari wa 7, ninaona mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika huko mbinguni kwa kutumia roho za malaika. Mapinduzi haya yalianza baada ya uasi wa shetani. Ndipo malaika kamanda mkuu Michaeli na jeshi lote la malaika wakapindua jeshi la lusifa huko mbinguni. Wokovu ukatangazwa mbinguni. Kisha mapinduzi yakafanyika pia Duniani alipokuja Bwana Yesu. Yeye mwenyewe akafanya mapinduzi kwa msalaba. Alipolia ELOI, ELOI, LAMASABAKTHANI; alifanya maombi ya mapinduzi yaliyompindua ibilisi na akasema IMEKWISHA katika Yohana 16:30. Agano la Kale likabadilika na kuunda Agano Jipya. Wakati pazia la hekalu linapasuka vipande viwili, Mungu alitenga Maagano mawili ukisoma Injili ya Mathayo sura ya 27 kuanzia mstari wa 45 hadi 54. Bwana Yesu hakuishia hapo, akasafiri safari ya mapinduzi kwenda kuzimu baada ya kumaliza hapa duniani. Huko kuzimu akamfunga lusifa na malaika waasi, akawaamisha waliokufa katika haki, ile paradiso akaihamishia juu mbinguni kama tunavyosoma katika mstari huu; ***"Na Tazama, pazia la HEKALU likapasuka vipande viwili toka juu hata chini, NCHI IKATETEMEKA, MIAMBA IKAPASUKA; MAKABURI YAKAFUNUKA, ikainuka MIILI MINGI YA WATAKATIFU WALIOLALA, nao wakisha kutoka makaburini mwao, baada ya KUFUFUKA kwake, wakaingia MJI MTAKATIFU [ PARADISO], wakawatokea wengi." [ MATHAYO 27: 51-53]***

## Aina za Mapinduzi

Swali lingine unaloweza kujiuliza wewe msomaji wa kitabu hiki linaweza kuwa kwa nini unahitaji Mapinduzi? Kwa sababu ya uvamizi wa shetani katika kizazi hiki kinachoitwa kizazi cha uzinzi. Shetani ameharibu mambo mengi kwa kuvamia maeneo mengi ya maisha yako, kabla hujazaliwa, maisha yako ya utotoni, maisha yako baada ya kuwa mtu mzima, maisha yako ya kusoma, maisha yako ya kazini, familia na maisha yako ya huduma mbalimbali. Umekuwa katika mpambano wa maisha magumu kwa muda mrefu sasa mpendwa! Lazima ufanye mabadiliko katika ulimwengu wa roho na mwili; Tangaza mapinduzi sasa; hakuna mtu mwingine wa kutangaza mapinduzi ya maisha yako. Ni wewe mwenyewe unatakiwa kutangaza mapinduzi kwa Jina lipitalo majina yote; Jina la Yesu Kristo! Naomba moyo wako sasa uanze kulipuka mapinduzi juu ya maisha yako! Moyo wako uwaze kufanya mapinduzi katika familia yenu; ukoo wenu; mtaani kwenu; kijijini kwenu; kwenye kata yako; kwenye tarafa yako; kwenye wilaya yako; kwenye mkoa wako; kwenye taifa lako! Ni wakati wa kupiga kelele za maombi ya maombolezo na sifa ili kuta za shetani zianguke. Kuna watu hawajui kuwa unaweza kuomba katika kelele za sifa; unaweza kuimba maombi ya sifa kwa muda mrefu na ngome zinaanguka. Hebu tazama Joshua katika kitabu cha Joshua sura ya sita mstari wa ishirini, Biblia inasema ***" Basi watu wakapiga kelele, na makuhani wakazipiga tarumbeta, hata ikawa, hapo watu waliposikia sauti ya tarumbeta haowa watu wakapiga kelele kwa sauti kuu sana, na ule ukuta wa mji ukaanguka nchi kabisa, hata watu wakapanda juu, wakaingia katika mji, kila mtu akiendelea kukabili mbele; wakautwaa huo mji"***.Yako maombi ya mapinduzi mengi yaliyofanyika katika sifa katika Biblia, unaweza pia kukumbuka Paulo na Sila walipoomba maombi ya sifa wakiwa gerezani; misingi ya gereza ilitetemeka na vifungo kukatika; utasoma kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya 16, mstari wa 25 na 26. Naomba utazame tena kitabu cha Mambo ya Nyakati wa pili, sura ya 20, kuanzia mstari wa 20 hadi 30. Mfalme Yehoshafati walivyobomoa ngome ya Wamoabu kwa maombi ya wimbo wa ***"mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema!"*** Maombi yako ya mapinduzi yafanyike kwa silaha kali za kiroho kama hizi; chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu; utashinda mpendwa.

Kila siku tunashuhudia katika vyombo vya habari vita kubwa inayoendelea duniani, shetani akipigana na wakristo. Wengine wanafikiri ni siasa tu, wengine wanafikiri kwamba kwa sababu za taaluma, kidiplomasia, kidemokrasia, na mgongano wa mawazo mbalimbali. Lakini mimi nakwambia huyu ni shetani mwenyewe anayetumia mawakala wake wanaomwabudu kufanya vita na wenye haki. Ndugu mpendwa, unahitaji mapinduzi ya vita inayoendelea kwa kutumia silaha ya maombi.

Mapinduzi yoyote yanayotokea, yawe ya kimwili au kiroho, hufanyika kimkakati, kwa kusudi la kuleta amani na furaha timilifu. Lakini maandalizi na gharama yake ni kubwa sana. Yako mapinduzi ya KIJESHI, la kiroho na kimwili pia, ambalo linahitaji maandalizi ya silaha na wanajeshi. Yako mapinduzi yanayofanywa kwa DEMOKRASIA, kama vile Tanzania tulivyopata uhuru wa bendera. Lakini pia kuna mapinduzi yanayofanyika kwa THEOKRASIA, yaani kwa kutumia uongozi wa Mungu. Theokrasia ni mpango wa Mungu katika uongozi na utawala wa watu wake hapa duniani. Mwandishi wa kitabu hiki, amezama zaidi katika mapinduzi yanayofanyika chini ya mpango huu wa Mungu.WOKOVU ni mapinduzi yaliyofanyika kwa mpango wa THEOKRASIA.UKOMBOZI wa Israeli ni mapinduzi ya KITHEOKRASIA yaliyofanyika katika ULIMWENGU WA ROHO NA MWILI. Katika kuhubiri kwangu injili ya mapinduzi katika miji na vijiji vilivyoko Tanzania, Afrika,Ulaya na Amerika, nimekuwa nikifunuliwa kufundisha kwamba, Ulimwengu wa Roho ndiyo unaoongoza Ulimwengu wa mwili. Ninao uthibitisho pia kibiblia pale Bwana Yesu alipofundisha kuwa roho i radhi mwili ni dhaifu katika mstari wa 41 sura ya 26 ya kitabu cha Mathayo Mtakatifu. Bwana Yesu alilisema neno hili wakati yuko kwenye maombi ya mapinduzi katika bustani ya Gethsemane. Roho ya Mapinduzi inaanza katika ulimwengu wa roho, kisha roho ya mapinduzi ikitawala ndipo mapinduzi hutokea. Kwahiyo,wanamapinduzi sharti watawaliwe kwanza na roho ya mapinduzi ndipo watafanikiwa kupindua roho zingine zilizokinyuma na mapinduzi. Wokovu ni mapinduzi na ni roho; Miujiza na ishara ni mapinduzi na roho; uhuru ni mapinduzi na roho; kuingia kwenye ndoa ni mapinduzi na ni roho; kutoka kwenye umasikini kwenda utajiri ni mapinduzi na roho; kuelimika na kutumia elimu kwa jili ya kuleta maendeleo ni mapinduzi; kufunguliwa mlango wa kiroho au kimwili ni mapinduzi na orodha ndefu unayoijua wewe msomaji wangu.

Mapinduzi yako au ya mtu binafsi yanayofanyika rohoni na maisha yake; familia, nyumba kwa nyumba, mtaa hata mtaa, kijiji hata kijiji, kata hadi kata, tarafa hadi tarafa, wilaya hadi wilaya, mkoa hadi mkoa, taifa hadi taifa, bara hadi bara. Baada ya kufanya mapinduzi watu husherehekea na kupiga tarumbeta kushangilia kazi iliyofanyika. Uhuru wa mtu binafsi na hata wa taifa unaleta furaha na maisha mapya. Bwana Yesu alipomaliza kuzipindua meza hekaluni na kutangaza matumizi ya hekalu, watu wote walikuwa wanashuhudia mapinduzi yale yakifanyika kwa halali, maana hakuna aliyemzuia kuzipindua meza; waliamua kumfuata hekaluni ili washiriki furaha yake ya ushindi huu. Biblia inasema hivi;

***"Na vipofu na viwete wakamwendea mle hekaluni, AKAWAPONYA. Lakini wakuu wa makuhani na waandishi walipoyoana maajabu aliyoyafanya, na watoto waliopaza sauti zao hekaluni, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi! walikasirika." [ MATHAYO 21: 14-15]***

Viwete kutembea, vipofu kuona, viziwi kusikia na wenye dhambi kutubu dhambi zao, ni mapinduzi ya ki-Mungu ambayo siyo tu watu wanapaza sauti zao kushangilia mapinduzi haya, bali hata malaika mbinguni wanashangilia. Lakini wapo wapinzani wa mapinduzi wanahofia nafasi zao na vyeo vyao katika mwili wa Kristo. Wakati huu inatisha kuwa walikuwa ni wakuu wa makuhani; ambao ni kama maaskofu wa sasa. Kama wewe ni askofu, usiogope unapoona mapinduzi yanafanyika katika huduma zingine, hasa zile za kiroho. Ni vibaya mchungaji kuanza kupinga kazi ya Mungu ndani ya mchungaji mwingine, kwa sababu hajawahi kuona miujiza na ishara zikifanyika katika huduma ile.

Mchungaji wa namna hii, anapingwa na Mungu pia kwa sababu

anampinga Mungu. Inatisha mchungaji wangu Mungu akianza kukupinga! Mwili wa Kristo Tanzania umeshambuliwa na adui kwa habari ya kuheshimu huduma za kiroho. Pamoja na kwamba wanasoma Biblia moja, wanashiriki Roho Mmoja, Wanaabudu Yesu Mmoja, Mungu Baba Mmoja. Hata shetani anatushangaa! Hata mataifa wanatushangaa! Siku moja nimepanda daladala; mpiga debe akawa anaongelea jinsi ambavyo wachungaji wa kiroho hawaelewani; na hata maaskofu hawaelewani; pale nilipokaa kwenye kiti nilipata shida baada ya kusikia mpiga debe anatoa ripoti kwa abiria waliokaa kwenye basi lile. Ndiyo, unaweza kuitafsiri hii ripoti kama ni ripoti ya shetani, kama ilivyokawaida ya wapendwa; lakini imebeba ukweli, ingawa kwa kuhukumu. Hili ni tatizo kubwa Tanzania, na ndilo linapelekea wachungaji Tanzania hasa wale wa kiroho kutopanuka katika huduma zao. Na wale waliopanuka kuanza kurudi nyuma kimavuno, kiuamusho na kiroho. Shetani ametushambulia na kutupuliza udini na miroromo ya ajabu, kiasi kwamba imefikia mahala, mchungaji anafunga na kuomba ili huduma ya mchungaji mwingine ife! Nasikia machozi ninapoandika habari hizi! Huduma ya Roho Mtakatifu, mchungaji wangu huwa haifi bali wewe utakufa utaiacha! Imekuwa kama watoto wanaogombania kiti kimoja cha utukufu, kila mmoja anataka aonyeshe kuwa huduma yake ni kubwa kuliko ya mwingine. Biblia inasema anayetaka kuwa mkubwa kuliko wengine na awe mdogo kuliko wote! Mchungaji, kubaliana na mimi unahitaji mapinduzi katika huduma yako, kwa muda ulioishi na vinyongo, huku unahubiri msamaha! Ni aibu mchungaji! Unahubiri msamaha wakati wewe hujasamehe! Unahubirije umoja wa kiroho wakati huna ushirikiano na huduma zingine? Unahubiri nini? Mungu siyo dhalimu kiasi hicho, akuletee watu wakati huna Upendo nao! Naomba Mungu afanye mapinduzi katika huduma yako katika Jina la Yesu! Bwana Yesu akufungulie milango 12 ya kufanya mapinduzi katika huduma yako, kuanzia sasa utapanuka ukianza kusamehe watumishi wenzako;Kuanzia sasa utaongezeka sana ukiwaheshimu wenzako. Amina, Mchungaji wangu!

Nchi yetu inawezakana inahukumiwa kwa sababu ya migongano na migogoro iliyoko katika mwili wa Kristo. Katika miaka ya karibuni kufikia mwaka 2003, baada ya mkutano wa Kwanza wa Kipentekoste kufanyika pale Mwenge katika Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship, ilionekana wapentekoste sasa wanaheshimiana, na wakasameheana kwa toba. Na Mungu alianza kuwafungulia milango mikubwa ndani ya nchi ya Tanzania na nje ya Tanzania, lakini pepo la dini na kiburi cha uzima likarudi tena kuanzia mwaka 2006 hadi sasa linaendelea kuutesa mwili wa Kristo. Hivi nikuulize mchungaji wangu, unafikiri Mungu anafurahi mbinguni kuona watoto wake, makuhani wake, wachungaji wake, mitume wake, manabii wake na walimu wake wanasemana vibaya na kuombeana vibaya? Hivi, unasomaje maneno ya Yakobo ya kwamba" *mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? na Aombe. Ana moyo wa kuchangamka? na aimbe zaburi [ YAKOBO 5:13].* Hivi unaweza kukataa kwamba hauhitaji ujumbe huu wa mapinduzi? Anza kufanya toba ili Mungu akufungulie milango ya mapinduzi. Kemea pepo la udini na kiburi katika Jina la Yesu! Kemea pepo la wivu katika Jina Yesu! Kemea pepo la masengenyo katika Jina la Yesu!

## Wokovu ni mapinduzi

Bwana Yesu alituma wanafunzi wake kufanya huduma hii kwa kuwapaka mafuta wangonjwa na wenye pepo, wote walifunguliwa; Tazama katika mstari huu:

***" Akawaita wale Thenashara, akaanza kuwatuma wawiliwawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu. Wakatoka, wakahubiri kwamba watu watubu. Wakatoa pepo wengi, WAKAPAKA MAFUTA watu wengi waliokuwa wagonjwa, wakawapoza."[ MARKO 6:7, 12-13]***

Bwana Yesu alipowatuma watumishi hawa kufanya huduma alijua ishara ya udhihirisho wa Roho Mtakatifu ni mafuta, ili watu wapate kuponywa. Mafuta ni alama ya uponyaji kutoka kwa nguvu za Roho Mtakatifu; kama unavyotumia mafuta ya kawaida kuponya vidonda katika ulimwengu

wa mwili. Kwa maana hakuna kinachofanyika katika ulimwengu wa Mwili ambacho hakikutokana na ulimwengu wa roho. Ulimwengu wa Roho ndiyo unaoongoza mambo yote tunayoyaona yanaendelea katika ulimwengu wa mwili.

Bwana Yesu alifanya tangazo la mapinduzi mara ya kwanza alipoanza huduma hekaluni katika Luka 4:18. Lakini kwa sababu kuna Mafarisayo ambao waliogopa mapinduzi walianza kutafuta jinsi ya kumhukumu ili kulinda nafasi zao. Kabla ya kuzaliwa kwake, kusulubiwa kwake, kifo chake, na kufufuka kwake; mapinduzi yalikuwa yakitangazwa tangu manabii na malaika kuanzia mwaka 1445 BC hadi 2000 AD, Baada ya Kristo, na hata sasa mapinduzi yanaendelea. Mbinguni mapinduzi yalifanyika kwanza kama inavyoelezwa katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana sura ya 12. Pale Msalabani mapinduzi yalifanyika kama inavyoelezwa katika kitabu cha Mathayo sura ya 26 hadi 27. Kule kuzimu mapinduzi yalifanyika kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Mathayo 28, Marko 16, Luka 24 na Yohana 20.

Kudhihirika kwake katika roho ya mapinduzi kule mbinguni, duniani na hata kuzimu ilikuwa ni kuzivunja kazi za ibilisi kama tunavyosoma katika waraka wa 1Yohana3:8. Lakini, kazi zote hizi zilifanyika na Bwana Yesu hasa hapa duniani kwa maombi yake ya mapinduzi usiku na mchana. Alitembea katika maombi, alifunga, alikesha, alilia na kuomboleza usiku na mchana. Siku moja, aliamua kwenda na wanafunzi wake, ambao ni mitume ;Yohana, Petro na Yakobo mlima wa maombi ya mapinduzi ili washuhudie mapinduzi yanayokuja mbele yao, katika kitabu cha Luka 9: 28-36. Sura yake iligeuka na kuwa ya malaika, wanamapinduzi wawili, Eliya na Musa walitokea kutabiri habari za mapinduzi atakayofanya. Wakati huu akina Petro, Yohana na Yakobo walikuwa bado hawajaelewa anaenda kufanya mapinduzi gani. Walijua Yesu anakwenda kufanya mapinduzi ya kisiasa katika nchi ya Israeli, kwahiyo walitegemea vyeo vya kisiasa atakapochukua utawala wa nchi. Unaweza kusoma habari kama hii katika kitabu cha matendo ya Mitume sura ya kwanza walipomwuliza swali hili:

***" Basi walipokutanika wakamwuliza, wakisema, Je, Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme? [ MATENDO 1:6]***

Katika historia ya mapinduzi yaliyofanyika kwa mkono wa Mungu, hakuna mpango ulioandaliwa ukashindwa. Tangu mwanzo hadi Ufunuo, ni habari za mapinduzi yaliyofanyika kwa Theokrasia kusababisha wokovu. Hivyo, tunaweza kusema BIBLIA kwa ujumla wote ujumbe wake mkuu ni WOKOVU. Kama ujumbe wake ni wokovu ambao ni mapinduzi ya maisha ya mwanadamu, tunaweza kusema BIBLIA NI KITABU CHA MAPINDUZI YA KIROHO.

## Miujiza na ishara ni Mapinduzi

Biblia kama kitabu cha miujiza na ishara, ni kitabu cha mapinduzi. Kazi ya ishara na miujiza ni kwanza kubatilisha kazi za ibilisi; Pili ni kwa ajili ya wasioamini wapate kuamini ya kwamba Yesu Kristo ni Bwana na Mwokozi. Miujiza ya Mungu wakati mwingine huigwa na shetani ili kubatilisha miujiza ya Mungu. Lakini kamwe miujiza ya Mungu haiwezi kubatilika hata kidogo, kwa sababu Mungu yuko juu ya yote, Yeye ni yote katika yote. Mungu anamtawala Shetani pia, Shetani naye anatawaliwa na Mungu, ndio maana alimhukumu tayari, ila anasubiri kunyongwa. Yawezakana wewe unayesoma kitabu hiki hujui shetani yuko wapi, na hatima yake ni nini. Shetani alitiwa gerezani huko kuzimu pamoja na malaika walioasi pamoja naye. Wako kifungoni hadi hapo Bwana Yesu atakaporudi, watafunguliwa muda mchache, kisha watanyogwa Jehanamu ya Moto. Unaweza kusoma habari katika kitabu cha 1 Petro 2:4. Bwana Yesu alipotawazwa kufanya mapinduzi duniani, alitangaza yeye mwenyewe hekaluni katika mistari hii:

***" Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia MAFUTA kuwahubiri maskini habari njema, Amenituma kuwatangazia wafungwa***

***kufunguliwa kwao; Na vipofu kupata kuona tena, na kuwaacha huru waliosetwa. Na kutangaza mwaka wa Bwana ulikubaliwa" [ LUKA 4:18]***

Hata leo, kazi hii ya mapinduzi inaendelea kwa sababu alichagua wanamapinduzi akawapaka mafuta kuwa Mitume, Manabii, Wainjilisti, Wachungaji na Waalimu. Katika Kanisa la Tanzania kuna hiyo hali ya kutotambuana na kuheshimiana kwa roho ya mapinduzi iliyoko juu wanampinduzi hawa. Lakini napenda kukwambia hata kama mchungaji hutambui na kuheshimu kati ya mitume, manabii, wainjilisti haimzuii Mungu kuwatumia kufanya mapinduzi. Nimekuwa nikuhubiri watu weusi na weupe, nakwambia kwamba Mungu hana mipaka katika kutenda kazi yake ya mapinduzi. Anaweza kutumia mtu yeyote katika mwili wa Kristo, ambaye hata maaskofu hawamtambui. Nakumbuka Paulo hakutambuliwa mara ya kwanza, kwa sababu kwanza yeye alikuwa katili kutekeleza matakwa ya Baraza la Sahedrin la kifarisayo. Pili, yeye siyo miongoni mwa wanafunzi, mitume wa Yesu waliokula , kunywa na kuitenda kazi pamoja naye. Tatu, huduma yake ilikuwa imevuka mipaka ya tamaduni za dini za kiyahudi; kwenda kuwahudumia mataifa. Kiutamaduni, Muyahudi hakuruhusiwa / alikua haruhusiwi kuchangamana na mataifa. Kwa sababu mitume walijua Yesu ni kwa ajili ya Wayahudi tu, itawezakanaje wokovu kwenda kwa mataifa?

Petro alipotambua ya kwamba Mungu ameshafanya mapinduzi ya ukabila na udini, alisema maneno haya: ***" Petro akafumbua kinywa chake, akasema, Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo, bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye."*** [ MATENDO10:34). Nakuomba mtu wa Mungu; anza kukubali kwamba Mungu anafanya mapinduzi na watu wake aliowachagua. Kama shetani anawatumia kufanya miujiza, mara nyingi Roho Mtakatifu atakufunulia si muda mrefu. Ndiyo, nakubali kuna sehemu ambapo shetani anaigiza miujiza, lakini muujiza wa Mungu shetani hawezi tenda wala kuigiza. Utakumbuka pale ambapo wachawi katika nyumba ya Farao walijaribu kuigiza miujiza aliyokuwa akifanya Musa. Fimbo ya Musa ilipogeuzwa kuwa nyoka, wachawi nao wakatengeneza nyoka. Lakini Biblia inasema, Nyoka wa Musa na Haruni aliwameza wote katika kitabu cha Kutoka 7:11-12. Biblia inasema nuru na giza havichangamani; wana wa nuru ni dhahiri na wana wa giza nao ni dhaihiri.

Na bado kuna tatizo pia katika huduma yako kama umehubiri miaka 3, 7, 5, 8, 9 10, 12, 15, 20, 21, 30 , 40, 50, 60, 67 hujawahi wewe mchungaji kushuhudia muujiza wowote wa Mungu unatendeka katika huduma yako. Kwa sababu mchungaji, miujiza inathibitisha Neno la Kristo unalowafundisha watu. Sasa nikwambie mtumishi, hiki kizazi kinataka ishara hata Bwana Yesu alisema. Wakati mwingine wasipoziona ishara, watakukimbia kwenda ambapo watapata miujiza. Watu hawataki hadithi na kelele nyingi, na fujo nyingi za kiroho, bila kuona matendo makuu ya Mungu! Na WEWE NI BALOZI WA MUNGU WA MIUJIZA! Ndiyo maana watu wanakimbilia kwa wachawi na waganga, ili waone hata hayo mazingaombwe na sarakasi za shetani. Mimi napenda kuwaambia wahubiri wa injili ya kwamba tusipotoa ushahidi wa Injili ya Yesu Kristo kwa miujiza na ishara, shetani atahubiri na kutoa ushahidi wa uongo kwa watu. Sasa hapa tusikasirike watumishi wa Mungu, maana watu hawaoni kitu kwetu, ni kelele tu! Injili ni ushahidi ya kwamba Yesu anaponya, hivyo hubiri uponyaji na Yesu ataponya! Ya kwamba Yesu anafungua vipofu, viwete, viziwi, mabubu na kufufua wafu; hubiri injili ya ushahidi huu na Bwana atafanya miujiza. Imani ya Yesu Kristo, inatakiwa ithibitishwe kwa Miujiza na Ishara kwa wasioamini wapate kuamini. Hii ni kazi yako wewe mchungaji, mwinjilisti, mwalimu, Mtume na Nabii; kwa sababu wewe ni balozi wa Yesu. Nikwambie mtumishi wa Mungu, watu wanayajua maandiko tangu utoto, na wanajua ukweli, ila wanahitaji kufunguliwa kutoka katika vifungo vya ibilisi kwa Jina la Yesu, ili Neno lithibitike kwa miujiza na ishara. Wewe, unafikiri kwa nini Musa hakutumwa na neno tu kwa Farao? Mungu alijua Farao na wachawi wake hawatakubali mpaka wayaone mapinduzi kwa miujiza na ishara. Injili ya Musa wakati huu haikuwa kama ya kwetu yenye kelele nyingi bila

matendo ya mapinduzi kwa ishara na miujiza; bali ilikuwa ni INJILI YA MAPINDUZI KWA MIUJIZA! HALELUJAH! MIUJIZA INAONGEA YENYEWE! MIUJIZA INAOKOA KATIKA JINA LA YESU!

Mtumishi mmoja alimwambia kwa kejeli Nabii mmoja ambaye ametumika zaidi ya miaka 67 katika huduma ya kimishionari kwa mataifa yote duniani; kwamba yeye haamini katika miujiza. Yule nabii akamwambia, ni sawa na yeye haamini katika miujiza, BALI ANAAMINI KATIKA MUNGU WA MIUJIZA. Yule mtumishi alishindwa kuendelea na maongezi na yule nabii, wakaachana! Mungu ni Mungu wa Miujiza! Inakuwaje wachungaji na maaskofu hawaamini katika Mungu wa Miujiza? Nadhani vyuo vya Theolojia inabidi vianze kufundisha na kuchanganua zaidi juu ya Miujiza ya Yesu kwanza ,kisha wafundishe maana ya miujiza na chimbuko la miujiza ya Mungu. Kusudi la Miujiza ni nini? Maana inaonekana wanafunzi ambao wamesoma na kubobea sana katika theolojia ni wagumu kutambua miujiza ya Mungu inayofanyika kuupindua ulimwengu wa giza. Na hasa miujiza inayofanyika chini mikono ya watumishi ambao hawajawahi kwenda vyuo vya Biblia. Lakini pia wanasahau kwamba shahada za Biblia na tunuku mbalimbali za falsafa wamezichukua kwa akina Petro Mtume aliyekuwa mvuvi wa samaki. Ingawa pia miujiza ya kutisha ilifanyika kwa mkono wa Petro, aliyekuwa mvuvi mvuvi wa samaki; alivua watu wengi kuingia katika ufalme wa Mungu kwa mkutano wake wa kwanza. Muujiza unapofanyika siyo tukio la kawaida, siyo sawa na kunywa panado kutuliza kichwa,ni Mungu mwenyewe anaingilia kati ndani mtu aliyefungwa na shetani katika upofu, uwete, ububu, uziwi, kifo na kufanya mapinduzi ya roho ya shetani, kisha Roho Mtakatifu anachukua nafasi. Hakuna hospitali yoyote ambayo inaweza kutibu UKIMWI, HAKUNA HOSPITALI YOYOTE INAWEZA KUFUFUA MAITI; HAKUNA DAKTARI AMBAYE NI BINGWA WA MIFUPA, ANAWEZA KUFANYA OPERESHENI KWA KIWETE, ANYOOSHWE MIFUPA ILIYOPINDA ISIMAME NA NYAMA ZIJAE , KISHA ATEMBEE!

Siyo kwamba sitambui huduma ya madaktari, lakini kuna mipaka ya huduma ya Daktari bingwa na Nabii wa Bwana. Kuna tofauti katika mapinduzi yanayoweza kufanyika kwa mikono ya mwanadamu na Mikono ya Mungu! Nakumbuka nilisafiri na madaktari bingwa wawili, mmoja wa mifupa na mwingine wa Saikolojia. Yule Daktari wa saikolojia akasema, lakini Biblia ni kitabu ambacho kimepitwa na wakati; Yule bingwa wa mifupa akasema, yeye anafanya kazi ya operesheni ya mifupa kwa muda mrefu na amesoma kuliko yule wa saikolojia; akasema kuna matukio nayona ndani ye Chumba cha upasuaji ambayo MKONO WA MUNGU UNAHUSIKA ASILIMIA 100. Akamwambia daktari mwenzake kwamba yeye ndiye yuko nyuma ya wakati kuliko Biblia. Mimi walinijua kuwa ni Mhubiri wa injili, lakini safari hii sikuongea lolote, maana Roho Mtakatifu aliniambia ameishamaliza kuhubiri kutumia daktari bingwa wa mifupa.

Roho wa Bwana anapokuwa juu yako, kama tulivyosoma maandiko katika mstari wetu Luka 4:18, lazima MAPINDUZI YA MATESO, MISIBA, MAGONJWA, FEDHA, ELIMU, MAISHA MAGUMU, MIGOGORO, KUKOSA MWELEKEO, MAADUI ZAKO, YATAKUJIA KATIKA JINA LA YESU WA NAZARETI! MWAKA HUU HAUPITI WEWE UNAYESOMA KITABU HIKI, MAPINDUZI LAZIMA YAKUTOKEE! SEMA AMINA! NA MILANGO 12 YA MAPINDUZI IFUNGUKE MBELE YAKO. MUNGU AKUPE MACHO NA UFAHAMU WA KUINGIA KATIKA MLANGO SAHIHI KATIKA JINA LA YESU! AMINA.